Serikali ya Canada yatoa Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya mwaka 2023

Kutekeleza mpango wa kiuchumi wa serikali ili kujenga uchumi imara unaomnufaisha kila mtu

Novemba 21, 2023 Ottawa, Ontario Idara ya Fedha ya Canada

Leo, Mheshimiwa Chrystia Freeland, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha, ametoa *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 202*3, akichukua hatua zaidi za kusaidia watu wa tabaka la kati la kiuchumi na kujenga nyumba zaidi kwa haraka zaidi.

Mpango wa kiuchumi wa serikali ni kujenga uchumi imara unaomnufaisha kila mtu, ikiwa ni pamoja na kazi au ajira nzuri ambazo watu wote nchini Canada wanaweza kuzitegemea. Na mpango huu tayari unatekelezwa.

Zaidi ya watu milioni moja nchini Canada wapo makazini hivi leo ikilinganishwa na kabla ya janga au mfumuko wa COVID-19. Mfumuko wa bei unaendelea kupungua, vipato au ongezeko la mishahara linakua kushinda mfumuko wa bei na sasa wachumi wa sekta binafsi wanatarajia Canada kuepuka mdororo wa uchumi kama ambavyo wengi walikuwa wametabiri.

Kutokana na ongezeko la haraka la viwango vya riba duniani, watu wengi nchini Canada wanakabiliwa na ugumu, hasa linapokuja suala la kumudu gharama za nyumba za kupanga au kununua nyumba. Katika kukabiliana na hali hiyo, *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 2023* inalenga katika kukabiliana na changamoto hizi kuu mbili hivi sasa.

Kwanza, serikali inaendelea kuwasaidia watu wote nchini Canada wakati huu ambapo bei za baadhi ya vitu bado zipo juu sana na vipindi vya kuingia upya kwa mikopo ya nyumba vinakaribia. Katika hatua mpya zilizolenga katika kudhibiti bei za vitu, kufanya gharama za maisha kuwa nafuu zaidi, na kuwalinda watu nchini Canada dhidi ya mikopo ya nyumba, serikali inachukua hatua za dhati kuwasaidia watu nchini Canada. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba watu wanapata unafuu kutoka kwenye mikopo ya nyumba wanaouhitaji katika kipindi cha viwango vya juu vya riba. Ili kutimiza hili, *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 2023* inatangaza Mkataba Mpya wa Mikopo ya Nyumba nchini Canada (Canadian Mortgage Charter), ambao unafafanua unafuu ambao watu nchini Canada wanaweza kutarajia kutoka kwa benki zao ikiwa wanakabiliwa na matatizo ya kifedha.

Pili, serikali inaongeza kasi ya kazi yake ya kujenga nyumba zaidi, kwa haraka, na kufanya gharama za makazi kuwa nafuu zaidi. Katika kuendeleza hatua kubwa ambazo serikali imekwishazichukua, *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 2023* inatambulisha mabilioni ya fedha katika ufadhili mpya wa kujenga nyumba zaidi na kwa haraka zaidi, serikali inachukua hatua kukabiliana na mikataba mifupi ya upangishaji ili nyumba zaidi zitumiwe na watu nchini Canada kuishi kitu ambacho kitasaidia kuongeza idadi ya wafanyakazi katika sekta

ya ujenzi nchini kote. Leo hii serikali kuu inaendelea kuongoza juhudi za kitaifa kufanya gharama za makazi kuwa nafuu zaidi kote nchini Canada.

Mpango wa kiuchumi wa serikali ni wenye uwajibikaji, na unahakikisha Canada inaendelea kuwa na viwango vya chini zaidi vya nakisi na deni kamili kwa uwiano wa GDP miongoni mwa nchi za G7. Serikali inachukua hatua zaidi katika *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 2023* kuhakikisha viwango vya fedha nchini Canada vinabaki kuwa endelevu—na kwamba tuweze kuendelea kuwekeza kwa uwajibikaji kwa watu wa Canada, kuimarisha tabaka la kati la kiuchumi, na kujenga uchumi imara unaomnufaisha kila mtu.

Kama sehemu ya msingi ya kazi ya serikali ya kuwekeza katika mustakabali wa kiuchumi wa Canada na kutoa nafasi zaidi za kazi zenye malipo mazuri, serikali pia inatoa kipaumbele katika utoaji wa misamaha mipya mikubwa ya kodi kwa uwekezaji, ambapo utekelezaji wa kisheria unaendelea katika siku zijazo na kuhitimishwa mwaka 2024

Nukuu

“Mpango wetu wa kiuchumi unahusu kujenga uchumi imara unaomnufaisha kila mtu, na *Taarifa hii ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe* ni hatua inayofuata ya mpango wetu. Kwa kuzingatia kuunga mkono tabaka la kati la kiuchumi na kujenga nyumba zaidi kwa haraka, tunachukua hatua kuhusu vipaumbele vinavyogusa watu wengi zaidi nchini Canada hivi leo - na tutaendelea kufanya kila tuwezalo kutoa huduma kwa watu wote kila pande ya nchini Canada.”

-Mheshimiwa Chrystia Freeland, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha

Ukweli wa Haraka

Mpango wa kiuchumi wa Canada unafanya kazi:

• Kiwango cha ukosefu wa ajira cha Canada, kwa miezi 21 iliyopita, kimekuwa chini kuliko wakati mwingine wowote chini ya serikali iliyotangulia. Zaidi ya watu milioni moja zaidi nchini Canada wana kazi au ajira hivi leo ikilinganishwa na kabla ya janga la COVID-19.

• Viwango vya mishahara vimezidi mfumuko wa bei kwa miezi tisa iliyopita.

• Shirika la Fedha la Kimataifa linatabiri Canada kuona ukuaji wa uchumi wenye nguvu zaidi katika kundi la G7 mwaka ujao.

• Kwa mujibu wa OECD, katika nusu ya kwanza ya mwaka huu, Canada ilipokea uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni wa tatu kwa wingi zaidi duniani - na wa juu zaidi kwa kila mtu (per capita) miongoni mwa mataifa ya G7.

Viunganushi Husika

• *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 2023*
• *Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe ya 2023*: Hatua Muhimu
• Maelezo ya Nyuma: Mpango wa Hatua za Makazi ya Canada
• Maelezo ya Nyuma: Kujenga Tabaka la Kati La Kiuchumi Linaloimarika
• Maelezo ya Nyuma: Kuwekeza kwa Wafanyakazi na Uchumi wa Canada Unaokua

Mawasiliano

Vyombo Vya Habari Vinaweza Kuwasiliana na:

Katherine Cuplinskas
Katibu wa Vyombo vya Habari na Mshauri Mwandamizi wa Mawasiliano
Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha
Katherine.Cuplinskas@fin.gc.ca

Mahusiano ya Vyombo vya Habari
Idara ya Fedha ya Canada
mediare@fin.gc.ca
613-369-4000

Maulizo ya Jumla
Simu: 1-833-712-2292
TTY: 613-369-3230
Barua Pepe: financepublic-financepublique@fin.gc.ca